**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU**

**-----------------**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA FUNGU 98 - WIZARA YA UJENZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

***[Imetolewa kwa mujibu wa Kanuni 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]***

**29 Mei, 2024**

**YALIYOMO**


**SEHEMU YA KWANZA** ........ 1

1.0 **UTANGULIZI** ........ 1

1.1 **Maelezo ya Awali** ........ 1

1.2 **Namna Kamati Ilivyotekeleza Majukumu Yake** ........ 1

**SEHEMU YA PILI** ........ 3

2.0 **UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024** ........ 3

2.1 **Maelezo ya Jumla** ........ 3

2.2 **Makusanyo ya Maduhuli** ........ 3

2.3 **Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida** ........ 5

2.4 **Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo** ........ 6

2.5 **Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo** ........ 7

2.6 **Changamoto za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo** ........ 15

**SEHEMU YA TATU** ........ 17

3.0 **MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025** ........ 17

3.1 **Umbile la Bajeti** ........ 17

3.2 **Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli** ........ 17

3.3 **Bajeti ya Matumizi ya Kawaida** ........ 18

3.4 **Bajeti ya Miradi ya Maendeleo** ........ 19

**SEHEMU YA NNE** ........ 21

4.0 **MAONI NA USHAURI** ........ 21

4.1 **Maoni ya Jumla** ........ 21

4.2 **Maoni Mahsusi** ........ 22

**SEHEMU YA TANO** ........ 28

5.0 **HITIMISHO** ........ 28

5.1 **Shukrani** ........ 28

5.2 **Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja** ........ 30

## VIFUPISHO NA MAANA

| | |
|---|---|
| **PPP** | Public Private Partnership |
| **TEMESA** | Wakala wa Ufundi na Umeme |
| **TANROADS** | Wakala wa Barabara Tanzania |
| **TANESCO** | Shirika la Umeme Tanzania |
| **TBA** | Wakala wa Majengo Tanzania |
| **EPC + F** | Engineering Procurement Construction Plus Financing |
| **O.C.** | Other Charges |
| **BRT** | Bus Rapid Transport |
| **CHICO** | China Henan International Cooperation Group |
| **CCECC** | China Civil Engineering Construction Cooperation |

## ORODHA YA VIELELEZO


**KIELELEZO NA. 1** MCHANGANUO WA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA KUFIKIA FEBRUARI, 2024

**KIELELEZO NA. 2** MCHANGANUO WA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MAENDELEO KUFIKIA FEBRUARI, 2024

**KIELELEZO NA. 3** ULINGANISHO WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**KIELELEZO NA. 4** ULINGANISHO WA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA 2024/2025

**KIELELEZO NA. 5** ULINGANISHO WA BAJETI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA 2024/2025

## SEHEMU YA KWANZA

# 1.0 UTANGULIZI

## 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inawasilishwa kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 na imegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo: -

a) **Sehemu ya Kwanza** ni Utangulizi na inaeleza kuhusu Msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake;
b) **Sehemu ya Pili** inatoa Uchambuzi na Tathimini ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;
c) **Sehemu ya Tatu** ni Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;
d) **Sehemu ya Nne** ni Maoni na Ushauri wa Kamati; na
e) **Sehemu ya Tano** ni Hitimisho.

## 1.2 Namna Kamati Ilivyotekeleza Majukumu Yake

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, hutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia

masharti mbalimbali yaliyoainishwa katika Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, katika kufanyia kazi utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilifanya yafuatayo: -

a) Kupokea taarifa na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 (Kanuni ya 117 (1));

b) Kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

c) Kupokea na kufanya uchambuzi wa Randama ya Wizara (Kanuni ya 115 (1)); na

d) Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, **Ibara ya 63 (3) (b)** ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inalipa Bunge madaraka ya kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa bajeti.[1] Aidha, Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti kwa Kamati za Kisekta kufanya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji na makadirio ya mapato na matumizi za Wizara kabla ya kujadiliwa Bungeni.[2] Kwa muktadha huo, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa **Fungu 98 - Wizara ya Ujenzi** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kufanya ulinganisho na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa mujibu wa **Kanuni ya 117 (2)**.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

a) Mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli
b) Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida
c) Utekelezaji wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

### 2.2 Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara ya Ujenzi iliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya **Sh.**

---

[1] Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977
[2] Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023

**70,000,000**. Hadi kufikia Februari, 2024 makusanyo ya maduhuli yalikuwa ni jumla ya **Sh. 142,368,000** sawa na **asilimia 203** ya malengo waliyojiwekea.

**Mheshimiwa Spika**, moja ya vyanzo vya makusanyo ya Wizara ni kazi za usajili wa magari mapya pamoja na uthamini wa magari chakavu. Kamati ilibaini kwamba makusanyo yalivuka lengo kwa sababu ya manunuzi yasiyotarajiwa ya magari na pikipiki kwa Fedha za Kupambana na UVIKO - 19 ambapo, magari mengi yalinunuliwa na kusajiliwa katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Januari 2024.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa makusanyo hayo ndani ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake Kamati imebaini kwamba, baadhi ya taasisi chini ya Wizara ya Ujenzi zinakabiliwa na changamoto ya kutopata fedha zitokanazo na huduma wanazotoa kwa taasisi nyingine za Serikali na hivyo kuathiri mwenendo wa makusanyo. Kwa mfano, Kamati imebaini kwamba, Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) hadi wakati inafanya tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya 2023/2024 madeni ambayo yamehakikiwa na kuwasilishwa kwa taasisi nyingine za Serikali yanafika **Sh. 39,463,035,862.33**. Kwa upande mwingine, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ilikuwa inazidai taasisi za Serikali **Sh. 2,250,954,983.82** ambapo hadi kufikia Desemba, 2023 ni **Sh. 85,122,000** tu zilikuwa zimelipwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa maoni ya Kamati, taasisi za Serikali kutolipa madeni kunakwamisha makusanyo ya taasisi hizo.

## 2.3 Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara iliidhinishiwa **Sh. 48,395,392,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Sh. 43,958,274,000** ni Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake na **Sh. 4,437,118,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2024, Wizara pamoja na taasisi zake zilikuwa zimepokea **Sh. 37,471,146,758.48**, sawa na **asilimia 77.43** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha zilizopokelewa, **Sh. 35,440,580,641.90** ni Mishahara **Sh. 2,030,566,116.58** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo kama ambavyo **Kielelezo Na. 1** kinafafanua.

**KIELELEZO NA. 1** – MCHANGANUO WA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA KUFIKIA FEBRUARI, 2024

| MATUMIZI YA KAWAIDA | BAJETI YA 2023/2024 (TZS) | MAPOKEZI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 (TZS) | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| MISHAHARA (P.E) | 43,958,274,000 | 35,440,580,641.90 | 80.62% |
| MATUMIZI MENGINEYO (O.C.) | 4,437,118,000 | 2,030,566,116.58 | 45.76% |
| **JUMLA** | **48,395,392,000** | **37,471,146,758.48** | **77.43%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na mapokezi ya jumla ya Fedha za Matumizi ya Kawaida. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutoa kwa wakati Fedha za Matumizi Mengineyo (O.C.) ili kuwezesha ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za kila siku za Wizara.

## 2.4 Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ilitengewa **Sh. 1,417,143,257,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Sh.1,081,966,569,000** ni Fedha za Ndani na **Sh. 335,176,688,000** ni Fedha za Nje. Fedha za Ndani zilijumuisha **Sh. 482,210,099,000** ambazo ni Fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **Sh. 599,756,470,000** ni Fedha za Mfuko wa Barabara.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2024, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Sh. 1,227,379,265,664.1** sawa na **asilimia 86**. Kati ya fedha hizo, **Sh. 892,202,577,664.12** ni Fedha za Ndani na **Sh. 335,176,688,000** ni Fedha za Nje. **Kielelezo Na. 2** kinatoa mchanganuo wa mwenendo wa mapokezi ya Fedha za Maendeleo.

**KIELELEZO NA. 2** – MCHANGANUO WA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO KUFIKIA FEBRUARI, 2024

| FEDHA ZA MAENDELEO | BAJETI YA 2023/2024 (TZS) | MAPOKEZI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 (TZS) | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| FEDHA ZA NDANI | 1,081,966,569,000 | 892,202,577,664.12 | 82.46% |
| FEDHA ZA NJE | 335,176,688,000 | 335,176,688,000 | 100% |
| **JUMLA** | **1,417,143,257,000** | **1,227,379,265,664.1** | **86%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi*

**Mheshimiwa Spika**, katika mapokezi ya Fedha za Ndani, Kamati imebaini kwamba Mfuko wa Barabara ulipokea **Sh. 459,613,828,432.38** sawa na **asilimia 76.63** ya **Sh. 599,756,470,000**

zilizoidhinishwa kwa Mfuko huo katika Mwaka wa Fedha 2023/2024.[3]

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na mwenendo wa mapokezi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo, na inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba, Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa zilitekeleza majukumu mbalimbali yakiwemo yafuatayo: -

a) Wizara kuanza kutumia Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Kazi pamoja na Miradi ya Maendeleo;
b) Ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja;
c) Ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT);
d) Ujenzi, upanuzi na ukarabati wa viwanja vya ndege;
e) Miradi ya Usalama Barabarani inayojumuisha shughuli za ujenzi wa mizani, na kufunga mifumo ya kupima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo;
f) Kununua na kujenga vivuko vipya, kukarabati vivuko vya zamani pamoja na kujenga maegesho ya vivuko; na
g) Ujenzi, ukarabati na usimamizi wa nyumba na majengo ya Serikali.

## 2.5 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, ili kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa baadhi ya

[3] Randama ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ya Fungu 98 – Wizara ua Ujenz, Uk. 16

miradi kati ya tarehe 12 na 17 Machi, 2024 katika mikoa ya Singida, Tabora, Shinyanga na Mwanza. Ziara hiyo ilifanywa ili kutimiza masharti kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1) kutathmini hali ya mapokezi ya fedha, hatua ya utekelezaji pamoja na kubainisha changamoto za utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitoe ufafanuzi wa miradi hiyo kwa muhtasari kama ifuatavyo: -

2.5.1 **Mradi Na. 4188 - Ujenzi wa Barabara (Noranga - Itigi)**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Ujenzi wa Barabara Kipande cha **Noranga – Itigi (Lot 7A)** chenye urefu wa **Kilometa 25** ni Sehemu ya Mradi Mkubwa wa Barabara ya **Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa** yenye jumla ya **Kilometa 413**. Kipande hiki kilianza kujengwa tarehe 16 Septemba, 2022 kwa lengo la kukamilika tarehe 01 Julai, 2024 baada ya tarehe ya awali ya kukamilika 16 Machi, 2024 kupita.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwa gharama ya **Sh. 29,770,297,741**. Mkandarasi wa Mradi ni Kampuni ya M/S China Henan International Cooperation Group Co. Ltd (CHICO) na Mshauri Elekezi ni M/S SABA Engineering PLC ya Ethiopia ikisaidiana na Kampuni ya M/S KAPSEL (T) Ltd ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, hadi wakati Kamati inatembelea eneo la Mradi kwa ukaguzi, maendeleo yalikuwa **asilimia 74.4** ukilinganisha na malengo ya kufikia **asilimia ya 97.24**. Aidha, Kamati ilitaarifiwa kwamba, tayari Mkandarasi wa

Mradi alikuwa amelipwa **Sh. 7,703,257,211.58** na malipo ambayo hayajalipwa ni **Sh. 8,911,234,348.72**, wakati Mhandisi Mshauri anadai **Sh. 500,136,300** kati ya **Sh. 1,693,240,000** za kazi ya ushauri elekezi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilihoji ni sababu zipi zilizosababisha Mradi kuchelewa kukamilika kwa wakati. Serikali ilitoa maelezo kwamba, utekelezaji wa mradi ulikabiliwa na changamoto ya mvua kubwa za El Nino zilizonyesha Novemba, 2023. Aidha, uwepo wa nguzo za umeme za TANESCO kwenye hifadhi ya barabara umechangia kuchelewa kwa mradi kwa sababu nguzo hizo zilitakiwa kuhamishwa na TANESCO kwa gharama ya **Sh. Bilioni 1.2**.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto hizo, Kamati imetaarifiwa kwamba, Serikali inaendelea na tathmini na uhakiki wa gharama na muda utakaotumika kuhamisha nguzo husika. Aidha, Serikali iko katika mchakato wa kumuongezea muda Mkandarasi ili kukamilisha kazi zilizobaki.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kwamba, wakati wa Maandalizi ya Miradi, ifanye upembuzi wa kina *(scoping)* kwa kushirikiana na taasisi za Serikali zinazohusika ili kuepukana na changamoto za kuongezeka kwa gharama za miradi kwa mabadiliko ya usanifu kwa uwepo wa miundombinu iliyowekwa na taasisi nyingine. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kutoa fedha za utekelezaji wa mradi wa **Barabara ya Makongolosi –**

**Rungwa – Itigi – Mkiwa** ili ukamilike mapema kwa kuzingatia umuhimu wa kuunganisha mikoa inayopitiwa na mradi huo.

2.5.2 **Mradi Na. 4159 – Ukarabati na Uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Tabora**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwa gharama ya **Sh. 24,626,767,735.34** (Bila VAT) ambapo ulianza tarehe 01 Aprili, 2023 na unatarajiwa kukamilika tarehe 11 Oktoba, 2024 kwa kuwa lengo la awali la kukamilika tarehe 31 Machi, 2024 halikufikiwa. Mkandarasi wa Mradi ni M/S Beijing Construction Engineering Group Co. Ltd, na Mhandisi Mshauri ni kampuni ya M/S Khatib & Alami Consulting Engineers – Offshore S.A.L. kutoka Lebanoni.

**Mheshimiwa Spika**, hadi wakati Kamati inatembelea Mradi huo, utekelezaji wake ulikuwa **asilimia 38** ukilinganisha na mpango kazi *(schedule of work)* wa kufikia **asilimia 43.6**. Aidha, Mkandarasi alikuwa tayari amelipwa malipo ya awali kiasi cha **Sh. 4,054,825,943.40** sawa na **asilimia 15** ya jumla ya gharama kimkataba *(total contract sum)*.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ulikabiliwa na changamoto mbalimbali zilizosababisha utekelezaji wake kuchelewa. Changamoto hizo ni pamoja na mvua kubwa zilizonyesha kati ya Novemba, 2023 na Februari, 2024. Aidha, uhamishaji wa miundombinu ya maji, umeme na mawasiliano kupisha mradi ulichelewa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kwamba, wakati wa kuingia mikataba na wakandarasi, iepuke kukubali mabadiliko ya gharama za mradi kutokana na sababu za hali ya hewa ikiwemo mvua kwa sababu, majira ya mvua katika nchi yetu yanajulikana.

### 2.5.3 Mradi Na. 4222 – Ujenzi wa Kiwanja wa Ndege cha Shinyanga

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwa gharama ya **Sh. 49,179,439,663**. Mkandarasi wa Mradi ni M/S China Henan International Cooperation Group Limited kutoka nchi ya China, na Mshauri Elekezi ni kampuni ya M/S SMEC International (PTY) Limited ya Australia ikishirikiana na SMEC (T) Limited.

**Mheshimiwa Spika**, mradi ulianza kutekelezwa tarehe 05 Aprili, 2023 kwa lengo la kukamilika ifikapo tarehe 04 Oktoba, 2024. Hadi wakati Kamati inatembelea ili kukagua mradi huo, utekelezaji wake ulikuwa ni **asilimia 10.4** ukilinganisha na malengo ya kufikia **asilimia 35.8.** Aidha, Kamati ilibaini kwamba, Mkandarasi alikuwa amelipwa **Sh. 7,930,184,645.66** kama malipo ya awali sawa na **asilimia 15** ya Mkataba. Vilevile, Mkandarasi alikuwa amewasilisha hati ya madai ya malipo ya **Sh. 2,698,485,934.53** ambayo TANROADS ilikuwa haijalipa bado.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto za uchelewashaji wa malipo kwa Mkandarasi, changamoto

nyingine ni pamoja na kuchelewa kwa uhamishaji wa miundombinu ya maji na umeme katika eneo la mradi pamoja na mvua kubwa zilizonyesha kati ya Novemba 2023 na Januari, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kumlipa Mkandarasi kwa wakati, na kumsimamia ili kiwanja hicho cha ndege kikamilike mapema na kuanza kutoa huduma kwa wakazi wa Shinyanga na mikoa ya jirani.

### 2.5.4 **Ujenzi wa Jengo la Makazi kwa Watumishi wa Umma, Eneo la Ghana, Mwanza, Block I**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kwa gharama ya **Sh. 6,192,260,778** ambapo ulianza tarehe 20 Januari, 2023 na unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 20 Julai, 2024. Hadi wakati Kamati inatembela mradi, ulikuwa umepokea **Sh. 2,123.159,500** sawa na **asilimia 34.28**. Aidha, utekelezaji wa mradi huo ulikuwa umefikia **asilimia 50**.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto kubwa inayoukabili mradi huu ni kutopatikana kwa wakati kwa fedha ili kuendana na kasi ya utekelezaji wake. Kamati inashauri kwamba, Serikali iiwezeshe TBA kupata fedha za kukamilisha mradi huu.

### 2.5.5 Mradi wa Ujenzi Kivuko pamoja na Maegesho ya Kivuko cha Buyagu – Mbalika, Mwanza

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) na unahusisha shughuli za ujenzi wa Kivuko Kipya cha Buyagu – Mbalika, pamoja na ujenzi wa maegesho yake. Gharama za ujenzi wa kivuko kipya peke yake ni **Sh. 3,817,064,000** ambapo Mkandarasi ni *Songoro Marine Transport Ltd* ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi ulianza tarehe 23 Aprili, 2023 na unatarajiwa kukamilika tarehe 04 Julai, 2024 ikiwa ni miezi minne (4) zaidi ya tarehe ya awali ya kukamilika mradi ambayo ilipaswa kuwa tarehe 28 Februari, 2024. Hadi wakati Kamati inafanya ukaguzi wa mradi huo, utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 45.9**. Aidha, Mkandarasi alikuwa ameshawasilisha hati za madai zenye thamani ya **Sh. 2,290,238,400** na malipo yaliyokuwa yamefanyika yalikuwa ni **Sh. 1,107,054,755** sawa na **asilimia 48.34** ya madai yaliyowasilishwa, na **asilimia 29** ya gharama yote ya mradi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Mradi wa Maegesho ya Buyagu – Mbalika, mradi unahusisha ujenzi wa maegesho upande wa Buyagu kwa gharama ya **Sh. 402,736,080** na ujenzi wa maegesho upande wa Mbalika kwa gharama ya **Sh. 574,510,800**. Hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba ujenzi wa maegesho hayo ulikuwa bado haujaanza, isipokuwa kazi zilizofanyika ni usanifu na taratibu za manunuzi tu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa miradi iliyokaguliwa. Moja kati ya changamoto hizo, ni Serikali kutopeleka fedha za kutosha na hivyo wakandarasi kucheleweshewa malipo. Changamoto nyingine ni ubovu wa barabara inayounganisha maeneo ambapo maegesho yatajengwa na maeneo mengine ya Wilaya za Sengerema na Misungwi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kwamba, Serikali itoe fedha za ujenzi wa **Kivuko cha Bulyagu – Mbalika** na kumlipa mkandarasi kwa wakati ili kivuko hicho kianze kutoa huduma katika Ziwa Victoria. Aidha, Serikali ijenge barabara ili kuwezesha wananchi wa maeneo ya kanda ya ziwa kufika katika maegesho ya kivuko hicho kwa urahisi.

### 2.5.6 Mradi Na. 4015 - Ujenzi wa Daraja la Kigongo – Busisi

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwa gharama ya **Sh. 592,608,692,836**, ambapo Mkandarasi ni China Civil Engineering Construction Corporation akishirikiana na China Railway 15 *Bureau Group Corporation (CCECC – CR15G JV)*.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ulianza kutekelezwa tarehe 25 Februari, 2020 kwa lengo la kukamilika tarehe 24 Februari 2024. Hata hivyo, kutokana changamoto mbalimbali, mradi unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 30

Desemba, 2024. Changamoto hizo ni pamoja na kuongezeka kwa kina cha maji ya Ziwa Victoria kulikosababishwa na mvua kubwa na hatimaye kubadilika kwa usanifu wa daraja. Changamoto nyingine ni mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 uliosababisha shughuli nyingi za kiuchumi kudorora.

**Mheshimiwa Spika**, hadi wakati Kamati inatembelea mradi, utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 85**, na tayari Mkandarasi alikuwa amelipwa **Sh. Bilioni 441.309** sawa na **asilimia 74.5**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ambayo mradi umefikia. Hata hivyo, ni vyema Serikali ikaongeza jitihada za kusimamia mradi huo ili ukamilike ndani ya muda wa nyongeza na kwa ubora unaostahili.

## 2.6 Changamoto za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mapokezi ya kuridhisha ya Fedha za Maendeleo, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali za utekelezaji wake zikiwemo zifuatazo: -

a) Uharibifu wa miundombinu ya barabara kutokana na mvua kubwa;
b) Malimbikizo ya madeni ya wakandarasi na wahandishi washauri katika miradi ya barabara; na
c) Uwezo mdogo wa Mfuko wa Barabara kugharamia matengenezo ya barabara kwa kuwa Mfuko huo unaweza kugharamia **asilimia 40.8** tu ya mahitaji halisi.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, tumeshuhudia mvua kubwa za El Nino ambazo kwa sehemu kubwa zimeharibu miundombinu ya barabara na madaraja nchini. Pamoja na jitihada zilizochukuliwa na Serikali kukabiliana na changamoto hiyo, Kamati imebaini kwamba, uwezo mdogo wa Mfuko wa Barabara kugharamia matengenezo ya barabara, unaathiri jitihada hizo kwa sababu matengenezo hayafanyiki kwa wakati na kwa kiwango kinachostahili.

**Mheshimiwa Spika**, aidha hadi wakati Kamati inakamilisha tathmini ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, miradi inayotekelezwa kwa utaratibu wa EPC + F ilikuwa haijaanza kutekelezwa kwa kuwa hakuna fedha iliyotolewa za kutekeleza miradi hiyo.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### 3.1 Umbile la Bajeti

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Ujenzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 1,708,958,532,000**. Kati ya fedha hizo, **Sh. 80,907,438,000** ni Matumizi ya Kawaida, na **Sh. 1,628,051,094,000** ni Fedha za Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, fedha inayoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa wastani wa **asilimia 22.13** ukilinganisha na Bajeti ya **Sh. 1,465,538,649,000** iliyotengwa kwa Mwaka wa Fedha unaoisha. **Kielelezo Na. 3** kinafafanua kwa muhtasari ulinganisho kati ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**KIELELEZO NA. 3** – ULINGANISHO WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

| BAJETI | MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | TOFAUTI (ASILIMIA) |
|---|---|---|---|
| MATUMIZI YA KAWAIDA | 48,395,392,000 | 80,907,438,000 | +67.18% |
| FEDHA ZA MAENDELEO | 1,417,143,257,000 | 1,628,051,094,000 | +14.88% |
| **JUMLA** | **1,465,538,649,000** | **1,708,958,532,000** | **+22.13%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi*

### 3.2 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Ujenzi inaomba kuidhinishiwa kukusanya maduhuli ya **Sh. 162,400,000** ambayo ni ongezeko **asilimia 132** ikilinganishwa na malengo ya makusanyo ya **Sh. 70,000,000** katika Mwaka wa Fedha unaoisha. **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali

kwa kuongeza makadirio yake ya makusanyo kwa kuwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha, makusanyo yalivuka malengo. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutathmini uwezo wake na hatimaye kubuni namna bora ya kukusanya kulingana na vyanzo vya mapato.

### 3.3 Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/205, Wizara ya Ujenzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 80,907,438,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Sh. 76,588,233,000** ni kwa ajili ya Mishahara na **Sh. 4,319,205,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C).

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa ujumla wake imeongezeka kwa **Sh. 32,512,046,000** sawa **asilimia 67.18** ukilinganisha na **Sh. 48,395,392,000** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama ambavyo **Kielelezo Na. 4** kinaonesha.

**KIELELEZO NA. 4** – ULINGANISHO WA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA 2024/2025

| MATUMIZI YA KAWAIDA | MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | TOFAUTI (ASILIMIA) |
|---|---|---|---|
| MISHAHARA (P.E.) | 43,958,274,000 | 76,588,233,000 | +74.23% |
| MATUMIZI MENGINEYO | 4,437,118,000 | 4,319,205,000 | -2.66% |
| **JUMLA** | **48,395,392,000** | **80,907,438,000** | **+67.18%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi*

**Meshimiwa Spika**, katika Fedha za Matumizi ya Kawaida, Mishahara imeongezeka kwa **asilima 74.23** wakati Fedha za Matumizi Mengineyo (O.C.) imepungua kwa **asilimia 2.66**.

Kamati ilitaarifiwa kwamba, ongezeko la Mishahara (P.E.) linatokana na ajira mpya, upandishaji wa vyeo, nafasi za uteuzi, mabadiliko ya kada za watumishi, pamoja na mabadiliko ya muundo wa baadhi ya taasisi zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza jitihada hizi za Serikali. Hata hivyo, Kamati ina maoni kwamba, ongezeko la Bajeti ya Mishahara linapaswa kwenda sambamba na ongezeko la Matumizi Mengineyo (O.C.) ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

### 3.4 Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 1,628,051,094,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo, **Sh. 1,081,966,369,000** ni Fedha za Ndani, na **Sh. 546,084,725,000** ni Fedha za Nje.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa wastani wa **asilimia 14.88** ukilinganisha na Bajeti ya **Sh. 1,417,143,257,000** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Ongezeko hilo linajionyesha katika **Kielelezo Na. 5**.

**KIELELEZO NA. 5** – ULINGANISHO WA BAJETI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA 2024/2025

| BAJETI YA MAENDELEO | MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | TOFAUTI (ASILIMIA) |
|---|---|---|---|
| **FEDHA ZA NDANI** | 1,081,966,569,000 | 1,081,966,369,000 | 0% |
| **FEDHA ZA NJE** | 335,176,688,000 | 546,084,725,000 | +62.92% |
| **JUMLA** | **1,417,143,257,000** | **1,628,051,094,000** | **+14.88%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, pamoja na kwamba Bajeti ya Maendeleo kwa ujumla wake imeongezeka katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali haijaongeza kabisa Fedha za Ndani katika Bajeti hiyo. Kwa kutotenga fedha za ndani kwa ajili ya kugharamia miradi ya Wizara ya Ujenzi, Serikali haionyeshi nia ya dhati ya kutekeleza miradi hasa kwa kuzingatia mahitaji makubwa ya miradi kama vile ya ujenzi wa barabara na madaraja nchini.

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya Kamati kuanza uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, ilibainisha mahitaji ya miradi ya ujenzi wa barabara nchini na kufanya kikao na Waziri wa Fedha ili kuitaka Serikali kutenga walau **Sh. Trilioni 5** Mwaka wa Fedha 2024/2025 ili kugharamia miradi hiyo. Kwa kuzingatia Bajeti iliyowasilishwa, Kamati haijaridhishwa na mwelekeo wa kibajeti kwa kuwa fedha zilizotengwa haziwezi kukidhi mahitaji yaliyopo.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI

### 4.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali ambayo kwa ufanisi mkubwa imeendelea kutoa fedha za kutekeleza majukumu mbalimbali ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi, hususan katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Katika kipindi cha miaka mitatu, Kamati imeshuhudia sehemu kubwa ya bajeti ya Sekta ya Ujenzi imekuwa ikitolewa kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha huo, na kwa kuthamini mtaji wa fedha za maendeleo unaotokana na kodi za wananchi, Kamati inaishauri Serikali ifanye yafuatayo: -

a) Kuongeza ufanisi na ubunifu katika utendaji kazi utakaochochea kuboresha huduma za Sekta ya Ujenzi nchini, kwa kuwa sekta hiyo ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi;

b) Kuongeza ufanisi na ubunifu katika kukusanya maduhuli kutokana na vyanzo vilivyopo, na kubaini vyanzo vipya ambavyo vitaongeza wigo wa makusanyo hayo. Sambamba na hilo, Serikali ihakikishe kwamba, huduma zitolewazo na taasisi zake, zinakuwa bora ili kukidhi matarajio ya wadau muhimu wa Sekta ya Ujenzi;

c) Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi yake yote ili iweze kuakisi viwango bora, uendelevu *(sustainability)* na kuwepo kwa thamani ya fedha *(value for money)*;

d) Wizara ya Fedha kutenga Kifungu Maalum ili iweze kukata Fedha za Matumizi ya Kawaida (O.C.) za Wizara mbalimbali kulingana na madai ya TBA, TEMESA na taasisi zingine za Serikali zinazotoa huduma kwa taasisi za Serikali ili kutozalisha madeni na kuzidumaza taasisi hizo; na

e) Serikali kulipa madai ya wakandarasi kwa wakati na madeni yaliyopo ili kuwezesha miradi kutekelezwa kwa wakati kupunguza kudaiwa riba na adhabu na kujenga imani mbele ya macho ya tasnia ya wakandarasi na wazabuni.

**Mheshimiwa Spika**, aidha Kamati inaishauri Wizara kuzisimamia taasisi zake kwa ukaribu zaidi ili kuhakikisha kwamba zinatekeleza majukumu yake yote kwa ufanisi. Kamati inaamini kwamba, iwapo kutakuwepo na usimamizi madhubuti, taasisi hizo zitaweza kujiendesha bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini na wakati huo huo zitaongeza tija na hatimaye kuboresha huduma za Ujenzi na kuongeza mapato ya Serikali.

## 4.2 Maoni Mahsusi

### 4.2.1 Wakala wa Majengo ya Serikali (TBA)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali, kufanya tathmini juu ya uwezo wa Wakala huu kujiendesha bila kutegemea ruzuku ya Serikali. Moja kati ya jitihada za msingi kufanyika, ni kuipa TBA mtaji wa kutosha, angalau **Sh. Bilioni 50** ili Wakala huo uanze kufanya uwekezaji mkubwa zaidi ambao utazalisha faida, na pia kushirikiana na Sekta Binafsi. Aidha, Wakala uruhusiwe kujenga, kuuza

na kupangisha nyumba zake kibiashara ili ipate mtaji wa kutosha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kubuni Mfumo mpya na rahisi utakaoiwezesha TBA kukusanya madeni, na iwapo taasisi za Serikali na wapangaji wengine watachelewa kulipa, mfumo huo uweze kutoza riba ya ucheleweshaji. Aidha, kwa taasisi za Serikali ambazo zinalipia Watumishi wake nyumba, na hawajalipa, basi TBA ichukue hatua stahiki ikiwemo kuwaondoa wadaiwa hao kwa kuwa mahitaji ya nyumba kwa Watumishi wa Serikali bado ni makubwa.

### 4.2.2 Matumizi ya Hifadhi ya Barabara

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, kwa mujibu wa sheria za nchi, hifadhi ya barabara za TANROADS inaweza kutumika kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi ambazo sio za kudumu. Kwa muktadha huo, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

a) Kutoa elimu kwa umma kuhusu Sheria zilizopo kuhusu fursa ya matumizi sahihi ya hifadhi ya barabara kwa shughuli za kiuchumi;
b) Kubainisha maeneo yenye mvuto wa kibiashara na kuyatangaza kwa umma ili yatumike kwa masharti maalum; na
c) Kuweka mifumo thabiti ya kukusanya fedha zitokanazo na matumizi ya hifadhi hiyo kwa viwango shindani kibiashara.

### 4.2.3 Serikali Kulipa Madeni ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, Serikali imekuwa ikisua sua katika kulipa madai na madeni ya wakandarasi na wahandisi washauri katika miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa barabara, ujenzi wa vivuko. Kwa Serikali kutolipa madeni hayo, kwanza kunakwamisha jitihada za kuwawezesha kiuchumi wananchi ambao wanapata changamoto ya marejesho ya mikopo katika taasisi za kifedha, lakini pia kunaathiri mzunguko wa fedha nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa sababu hizo, Kamati inaishauri Serikali kuwa na mkakati madhubuti na wa kudumu ili kulipa madeni kwa wakati lakini pia kuwajengea uwezo wakandarasi wa ndani ili watekeleze miradi mingi zaidi.

### 4.2.4 Fidia kwa Wananchi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, baadhi ya wananchi katika maeneo mbalimbali nchini ambao waliachia maeneo yao ili kupisha miradi inayosimamiwa na Wizara ya Ujenzi bado hawajalipwa fidia.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, wananchi wote wanaodai fidia, walipwe stahiki zao kwa mujibu wa sheria na iwapo Serikali haina uwezo wa kulipa fidia katika maeneo waliyotwaa, maeneo hayo yarejeshwe kwa wananchi.

4.2.5 **Mkakati wa Kuondoa Matuta Ambayo si ya Lazima**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kwamba, Serikali katika kudhibiti mwendokasi wa madereva imeweka matuta katika maeneo mbalimbali nchini. Hata hivyo, Kamati inashauri kwamba, Serikali ifanye tathmini ili kubainisha maeneo ambayo hakuna umuhimu wa kuwepo matuta na iwapo maeneo hayo yana matuta, basi yaondolewe. Ushauri huu umejengwa katika misingi kwamba, uwepo wa matuta una athari hasi za kiuchumi kwa watumiaji wa magari. Hata hivyo, kwa yale maeneo ambayo kuna ulazima wa matuta kuwepo, matuta hayo yawe na viwango stahiki na vinavyolingana nchi nzima.

4.2.6 **Mkakati wa Kujenga Mizani Inayopima Magari Yakiwa Katika Mwendo**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuendelea kukabiliana na changamoto ya uzito wa magari uliopitiliza na ambao unaharibu barabara nchini, Kamati inashauri kwamba, pamoja na vituo vya mizani vilivyopo, Serikali pia ijenge Mizani inayopima magari yakiwa katika mwendo. Hatua hii itaongeza jitihada za Serikali kudhibiti uzito wa magari maeneo mengi zaidi nchini.

4.2.7 **Ujenzi wa barabara za mwendo wa haraka *(Express Ways)***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kushauri kwamba, ili kukabiliana na changamoto za msongamano wa magari hususan katika barabara zinazoingia miji mikubwa nchini, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ibuni miradi

ya ujenzi ya barabara za mwendo wa haraka *(express ways)*. Aidha, Serikali inashauriwa kujenga barabara hizo kwa kushirikiana na sekta binafsi (PPP) na kuweka tozo za matumizi yake *(road tolls)*.

4.2.8 **Ujenzi wa Barabara kwa Utaratibu wa EPC + F**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Kamati imebaini kwamba miradi iliyopaswa kutekelezwa kwa utaratibu wa EPC + F haijatekelezwa kabisa, Serikali ifanye tathmini kuhusu utaratibu huo kuona iwapo una tija.

4.2.9 **Maboresho ya Utendaji wa TEMESA**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Kamati imebaini kwamba, pamoja na kwamba Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) inatoa huduma za matengenezo ya magari ya Serikali, wakala huo unakosa ufanisi kwa sababu ya kuwepo kwa changamoto ya madai na madeni. Kwa muktadha huo, Kamati inashauri kwamba, Serikali ibuni Mfumo wa Kielektroniki ambao utaweka utaratibu kwamba, baada ya gari la umma kubainika kuwa na tatizo la kiufundi *(diagnosis)*, taarifa zake zitumwe katika taasisi husika na gharama za matengenezo yake, na gari hiyo isitengenezwe hadi hapo taasisi husika itakuwa imekamilisha malipo.

4.2.10 **Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza jitihada za Ujenzi wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Jijini Dar es Salaam. Pamoja na hayo, Serikali inashauriwa kuharakisha mradi huo na kuboresha miundombinu inayozunguka

mradi huo hasa mifereji ya maji ili kuepuka changamoto zinazowakabili watumiaji wa barabara wakati ujenzi huo unaendelea.

### 4.2.11 Kutunisha Mfuko wa Barabara

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, uwezo wa Mfuko wa Barabara kukarabati barabara nchini ni mdogo ukilinganisha na mahitaji halisi kama ambavyo taarifa hii imefafanua hapo awali. Aidha, kwa kuwa mahitaji ya ukarabati wa barabara nchini yanaongezeka, Kamati inashauri Serikali itafute vyanzo vipya vya mapato ambavyo vitawezesha Mfuko wa Barabara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

**SEHEMU YA TANO**

# 5.0 HITIMISHO

## 5.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee naendelea kukushukuru wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu na kwa maelekezo yako ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za kila siku za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Aidha, namshukuru Naibu Spika, kwa namna anavyokusaidia kutekeleza majukumu yako, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuendesha kwa ufanisi Vikao vya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa moyo wa dhati kabisa, niwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuendelea kuisimamia Wizara ya Ujenzi pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa niaba ya Bunge lako tukufu. Kwa hakika, maoni, ushauri na mapendekezo yao vina mchango mkubwa katika kuboresha utendaji wa Serikali. Naomba niwatambue Wajumbe hao ili majina yao yaingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Moshi Selemani Kakoso, Mb. | **Mwenyekiti** |
| 2. | Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb. | **Makamu** |
| 3. | Mhe. Kapt. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb. | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo, Mb. | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Abubakar Damian Asenga, Mb. | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb. | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Ally Anyigulile Mlaghila Jumbe, Mb. | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| 8. | Mhe. Amina Ali Mzee, Mb. | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Angelina Adam Malembeka, Mb. | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Fredrick Edward Lowassa, Mb. | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mb. | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb. | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Innocent Edward Kalogeris, Mb. | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako Mb. | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Livingstone Jpseph Lusinde, Mb. | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Mbarouk Juma Khatib, Mb. | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mb. | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Mohamed Maulid Ali, Mb. | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mb. | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Mwatumu Dau Haji, Mb. | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Stella Simon Fiyao, Mb. | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Sylvia Francis Sigula, Mb. | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Ujenzi, Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, (Mb) kwa ushirikiano ambao ameipatia Kamati katika kipindi chote cha Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati akisaidiwa na Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhe. Mhandisi Godfrey Msongwe Kasekenya (Mb).

Aidha, niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi pamoja na taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Balozi Mhandisi Aisha Amour. Kamati inatambua mchango wa watendaji hao katika maendeleo ya Sekta ya Ujenzi na inaendelea kuwatia moyo kwamba wafanye kazi kwa bidii.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru sana watendaji wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Bi. Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc* kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

5.2 **Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Moshi Selemani Kakoso, Mb.

**MWENYEKITI**

**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu**

29 Mei, 2024